## HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOZI

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, MIPANGO NA UONGOZI (KAWAIDA) KILICHOFANYIKA TAREHE 21/01/2022 KATIKA

## UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA – MBOZI

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. G.J. Musyani | - | Diwani Kata ya Nanyala | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. C. M. Kibona | - | Diwani Kata ya Hasamba | - | Mjumbe |
| 3. | Mhe. T. T.Nzunda | - | Diwani Kata ya Nyimbili | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. M. Mwashitete | - | Diwani Kata ya Halungu | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. S.T. Nzunda | - | Diwani Kata ya Itumpi | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. S . Mbwaga | - | Diwani Kata ya Isansa | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. F. L. Kibona | - | Diwani V/Maalum | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. D. Mboya | - | Diwani Kata ya Mlangali | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. B. Sinienga | - | Diwani Kata ya Ipunga | - | Mjumbe |
| 10. | Bw.Abdallah H. Nandonde | - | Mkurugenzi Mtendaji (W) | - | Katibu |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. J.N. Hasunga | - | Mbunge Jimbo la Vwawa | - | Kwa taarifa |
| 2. | Mhe. G. R. Mwenisongole | - | Mbunge Jimbo la Mbozi | - | Kwa taarifa |

**WATAALAM WALIOKUWEPO:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 01. | Bi. Tusubilege Benjamin | - | Katibu Tawala (W) |
| 02. | Bw. Raphael Makoninde | - | Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala |
| 03. | Bw. Erasto mwasanga | - | Mkuu wa Idara ya Mipango |
| 04. | Bw. Danford Mwelelwa | - | Mkuu wa Idara ya Mifugo Na Uvuvi |
| 05. | Bi. Melania Kwai | - | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 06. | Bw. Emmanuel Masele | - | Mkuu wa Idara ya Fedha |
| 07. | Bw. Mwasa Waziri | - | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani |
| 08. | Bw. Danny Tweve | - | Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi |
| 09. | Bw. Saidi M. Ngondo | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 10. | Bw. Charles Joseph | - | Mhandisi |
| 11. | Bw. Oscar Mgani | - | Mtendaji Mamlaka ya Mji Mdogo Vwawa |
| 12. | Bw. Lazaro Mwakimenya | - | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha sheria |
| 13. | Bw. Joel Kaminyoge | - | Mtendaji Mamlaka ya Mji Mdogo Mlowo |
| 14. | Bw. Charles Ndimbwa | - | Mkuu wa Kitengo cha Nyuki (W) |
| 15. | Bw. Richard Mwailanga | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo |
| 16. | Dr. Mponjoli Nelson | - | Mkuu wa Idara ya Afya |
| 17. | Bw. Laurent E. Nyalugulu | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi Na Maliasili |
| 18. | Bw. Baraka Bunzu | - | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ugavi |
| 19. | Bw. Abihud Fungamtama | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 20. | Bw. Michael Mbeyanje | - | Kaimu Mratibu wa kudhibiti Ukimwi |
| 21. | Bw. Hamis P. Nzunda | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mazingira |

**SEKRETARIETI:**

1. Bw. F. Mwashibanda - Mwandishi wa Vikao H/W
2. Bi. D. Pwele - Mwandishi wa Vikao H/W

**MUHT.NA.KF/MBZ/01/01/2022:- KUFUNGUA KIKAO**

Katibu aliomba radhi kwa kutoshiriki kikao cha kamati ya fedha, Mipango na Uongozi (bajeti) ni kutokana na kupata ugeni wa Naibu Waziri Utumishi. Akifungua kikao Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe na Wataalam kwa kuhudhuria na kueleza kuwa ni kikao cha kawaida. Baada ya utangulizi huo alifungua kikao mnamo saa 03:20 asubuhi.

**MUHT.NA.KF/MBZ/02/01/2022:- KURIDHIA AGENDA**

Agenda za kikao cha Kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi cha tarehe 21/01/2022 zilisomwa na kuridhiwa kama ifuatavyo;-

01. Kufungua kikao
02. Kuridhia agenda
03. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao kilichopita cha Kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi cha tarehe 17/12/2022
04. Yatokanayo na Kikao kilichopita cha Kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi cha tarehe 17/12/2022
05. Taarifa ya mapato na matumizi kuishia Disemba, 2021
    a) Halmashauri ya Wilaya
    b) Mapato ya Kata kuanzia Julai, 2021 – Disemba, 2021
06. Mapokezi ya fedha za Halmashauri ya Wilaya mwezi Disemba, 2021
07. Tathimini ya ziara ya Kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi.
08. Taarifa ya Mkaguzi wa Ndani robo ya pili 2021/2022
09. Taarifa ya Miradi ya Maendeleo robo ya pili 2021/2022
10. Taarifa ya Kitengo cha Manunuzi robo ya pili 2021/2022
11. Taarifa ya Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF) robo ya pili 2021/2022
12. Taarifa ya utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa udhibiti wa vihatarishi robo ya pili 2021/2022
13. Taarifa ya marekebisho ya vifungu (Reallocation) katika bajeti ya Mwaka 2020/2021
14. Taarifa ya kila mwezi:
    a) Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)
    b) VVU na UKIMWI.
    c) Utekelezaji wa shughuli za Idara ya Utawala na Utumishi.
15. Taarifa za Mkurugenzi.
16. Kufunga Kikao.

**MUHT.NA.KF/MBZ/03/01/2022:- KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA.**

Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi kilichopita cha tarehe 17/12/2021 ulisomwa na kuridhiwa na Wajumbe kisha kuwekwa saini na Mwenyekiti pamoja na Katibu kuwa kumbukumbu sahihi za Halmashauri.

**MUHT.NA.KF/MBZ/04/01/2021:- YATOKANAYO NA KIKAO KILICHOPITA**

**Yatokanayo Na. 1 lililohusu** kutoa elimu kwa jamii ili kubadili mtazamo na kutumia tofali za saruji wajumbe walishauri yafuatayo;

- Idara ya mazingira waongeze usimamizi wa Sheria kwa wanaofyatua tofali mbugani ili tofali za Block zipate wateja.

**Yatokanayo Na. 3 lililohusu** Mafundi waliokimbia na fedha za mradi wa ujenzi zahanati ya Mtunduru kiasi cha Tsh.1,800,000/= wafuatiliwe ili fedha zirejeshwe kukamilisha mradi, wakijadili Wajumbe walishauri katika utekelezajiwa miradi ya maendeleo ushirikiano baina ya Wataalam na Wah. Madiwani uimarishwe.

**Yatokanayo Na. 4 lililohusu** ukusanyaji wa madeni ya wakusanya mapato wajumbe walishauri kuwa Mikakati iongezwe na kufuatilia madokezo kwa wale wanaodai fedha Halmashauri ili walipwe.

**AZIMIO;**

- Menejimenti ifanye jitihada za kukutana na uongozi wa Kampuni ya GDM na kufanya mazungumzo ili deni la **Tsh. 57,534,630.00** wanalodaiwa lilipwe na taarifa iwasilishwe kikaoni Yatokanayo na kikao kilichopita yaliwasilishwa kwa Wajumbe na kujadiliwa na kupokelewa.

**MUHT.NA.KF/MBZ/05/01/2022:-TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KUISHIA DISEMBA, 2021.**

**UTANGULIZI:**

Ilielezwa kwamba kwa Mujibu wa Kanuni na Taratibu za uendeshaji wa Halmashauri, kila mwezi Halmashauri inatakiwa kuandaa taarifa ya mapato na matumizi yake na kuiwasilisha katika mamlaka mbalimbali kwa wananchi ili kujua mwenendo wa mapato na matumizi katika Halmashauri yao kisha kuwasilisha taarifa ya utendaji wa ukusanyaji mapato na matumizi kwa mwezi Novemba, 2021 robo ya pili ya mwaka inayoishia tarehe 31 Disemba, 2021.

**Malengo Mahususi ya Halmashauri.**

- Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa mujibu wa bajeti ya **Tshs 3,189,570,027.60** na mapato ya ruzuku toka Serikali Kuu kwa mujibu wa bajeti **Tshs 51,789,784,606.00** na kufanya jumla ya mapato yaliyoidhinishwa na Baraza la Madiwani pamoja na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ,Kanuni na Miongozo ya fedha kuwa **Tshs. 54,979,354,633.60** ifikapo June 30, 2022

- Kusimamia matumizi ya vyanzo vya ndani na matumizi ya ruzuku toka Serikali kuu kwa mujibu wa bajeti **Ths 54,979,354,633.60** iliyoidhinishwa na baraza la madiwani pamoja na Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria,Kanuni na Miongozo ya fedha ifikapo Juni 30, 2022.
- Kupeleka huduma kwa wananchi kwa mujibu wa Bajeti iliyoidhinishwa na Baraza la Madiwani na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ifikapo Juni 30,2022.

**MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI.**
**UKUSANYAJI MAPATO.**
**MAPATO YA NDANI**

Ilielezwa kwamba kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri iliidhinishiwa kukusanya mapato ya ndani kiasi cha **Tshs 3,189,570,027.60** kati ya mapato hayo **Tshs 2,724,731,273.60** ni mapato ya ndani halisi na **Tshs 464,838,754.00** ni mapato ya kisekta. Vilevile iliidhinishiwa kupokea mapato toka Serikali Kuu na wahisani **Tshs 51,789,784,606.00** kufanya jumla ya Makisio kwa mapato yote kuwa **Tshs 54,979,354,633.60.**

Ilielezwa kwamba kwa mwezi wa Disemba, 2021 Halmashauri imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Tshs 386,669787.95** ya mapato ya ndani halisi na Mapato ya Kisekta **Tshs 46,700,000.00** na hivyo kufanya jumla ya makusanyo ya mapato ya ndani Halisi, na ya kisekta kwa mwezi Disemba,2021 kuwa **Tshs 433,369,787.95**.

Ilielezwa kwamba kuanzia mwezi Julai – Disemba, 2021 Halmashauri imekusanya jumla ya kiasi cha **Tsh 2,089,271,201.95** Kwa mapato halisi Sawa na asilimia **153.36** ya lengo la Julai – Disemba,2021 na asilimia **76.68** ya lengo la mwaka. Kwa upande wa mapato ya kisekta imekusanya Tshs **300,401,000** sawa na asilimia 129.23 la lengo la Julai- Disemba, 2021 na asilimi **64.62** ya lengo la mwaka na hivyo kufanya jumla ya Mapato ya Ndani halisi na Kisekta **Tsh 2,389,672,201.95** Sawa na asilimia **149.84** ya lengo la Julai – Disemba na asilimia **74.92** ya lengo la mwaka.

**MAPATO YA RUZUKU TOKA SERIKALI KUU NA WAHISANI**

Ilielezwa kwamba kwa mwezi wa Disemba, 2021 Halmashauri imefanikiwa kupokea kiasi cha **Tshs 3,253,834,396.7** ya mapato ya matumizi ya kawaida na Mishahara, **Tshs 875,817,841.52** kama mapato kwa ajili ya Miradi ya maendeleo, na hivyo kufanya Jumla ya mapato ya ruzuku toka Serikali Kuu na wahisani kuwa **Tshs 4,129,652,238.22.**

Hivyo kuanzia kipindi cha Julai – Disemba, 2021 Halmashauri imepokea jumla ya kiasi cha **Tsh 21,093,831,548.78** kama Mishahara na matumizi ya kawaida Sawa na asilimia **101.33** ya lengo la Julai –Disemba na asilimia **50.67** ya lengo la mwaka na imepokea jumla ya **Tshs 5,621,819,523.52** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia **110.41** ya lengo la Julai- Disemba, 2021 na aslimia **55.20** ya lengo la mwaka; hivyo kufanya jumla ya mapokezi ya ruzuku na wahisani kuwa **Tshs 26,715,651,072.30** sawa na asilimia **103.11** na Julai- Disemba na asilimi **51.56** ya

lengo la mwaka na hivyo kufanya jumla ya Mapato yote kuwa **Tsh 29,105,323,274.25** sawa na asilimia **105.48** ya lengo la Julai – Disemba na asilimia **52.74** ya lengo la mwaka.

**MATUMIZI.**

**MATUMIZI YA MAPATO YA NDANI.**

Ilielezwa kwamba kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ilikisia kutumia mapato halisi ya ndani **Tshs 2,724,731,273.60** na mapato ya kisekta ilipanga kutumia **Tshs 464,838,754.00** na kufanya jumla ya Makisio ya Matumizi kutoka mapato ya ndani kuwa **Tshs 3,189,570,027.60.**

Pia ilielezwa kwamba kwa mwezi Disemba 2021, Halmshauri imetumia Jumla ya **Tshs 448,373,380.03** kati ya **hizo 200,754,338.16** kwa matumizi ya kawaida, **Tshs 200,919,041.87** kwa matumizi ya Miradi ya Maendeleo na **Tshs 46,700,000.00** kwa Matumizi ya Kisekta.

Hivyo kwa kipindi cha Julai- Disemba,2021 Halmashauri imetumia jumla ya kiasi cha **Tshs 1,688,876,045.04** sawa na asilimia **105.90** ya lengo la Julai – Disemba na asilimia **52.95** ya lengo la mwaka; kati ya hizo **Tshs 768,246,803.17** kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia **93.98** ya lengo la Julai – Disemba na asilimia **46.99** ya lengo la mwaka, **Tshs 620,228,241.87** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia **113.81** ya lengo la Julai-Disemba na asilimia **56.91** ya lengo la mwaka na **Tshs 300,401,000** sawa na asilimia **129.25** ya lengo la Julai-Disemba na asilimia **64.62** ya lengo la mwaka kwa ajili ya matumizi ya kisekta.

**MATUMIZI YA RUZUKU TOKA SERIKALI KUU NA WAHISANI.**

Ilielezwa kwamba Halmashauri ilikisia kutumia kiasi cha **Tshs 2,609,028,560.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida, **Tshs 38,996,886,000.00** kwa ajili ya mishahara, na **Tshs 10,183,870,046.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Ilielezwa kwamba Kwa mwezi Disemba, 2021 Halmashauri imetumia kiasi cha **Tshs 4,180,077,522.38** kwa ajili ya matumizi ya kawaida, Mishahara na Miradi ya Maendeleo.

Hivyo kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 31, 2021 Halmashauri imetumia **Tshs 24,839,170,373** kwa ajili ya matumizi ya kawaida,Mishahara na Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia **90.4** ya lengo la Julai – Disemba na asilimia **45.2** ya lengo la mwaka.

**MAFANIKIO**

- Halmashauri imefanikiwa kukusanya mapato ya ndani kwa asilimia **149.84** ya lengo lake la miezi sita.
- Halmashauri imefanikiwa kupokea asilimia **103.11** ya fedha toka Serikali Kuu na wahisani.

**CHANGAMOTO.**

- Wakusanya mapato kutokuweka fedha benki kwa wakati.
- Kukosekana kwa elimu ya umuhimu wa kulipa ushuru na Sheria, Kanuni na Taratibu za usafirishaji mazao.
- Wafanyabiashara wa leseni kuchukua vitambulisho vya ujasiliamali.
- Kutorosha/ kukwepa kulipa ushuru hasa wakati wa usiku.
- Baadhi ya vyanzo kukusanywa kwa Msimu

**6.0.MAPENDEKEZO.**

- Kuwahamasisha wakusanya mapato wanaopatikana maeneo yenye huduma za kibenki kuzibenki fedha hizo kila siku, kwa wale walioko mbali na Halmashauri watumiwe Control number na wale wasio kwenye huduma za kibenki wabenki fedha hizo kwa njia ya mpesa,tigo pesa ,na halotel money nk.
- Kuendelea kutoa elimu ya umuhimu wa kulipa tozo mbalimbali za serikali.
- Kutoa elimu kwa wafanyabiashara wakubwa wenye vitambulisho vya mjasiliamali ili waweze kulipa mapato ya serikali.
- Kufanya doria za mara kwa mara usiku ili kupata mapato yanayotoroshwa
- Kuendelea kukusanya kwa makini kwa vyanzo vyote vya mapato vinavyokusanywa kwa msimu.

**.MAPATO YA KILA KATA MWEZI DISEMBA, 2021.**

Ilisomwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri imekisia kukusanya **Sh. 2,549,071,102.98** kutoka kwenye kata **29.** Hadi kufikia 30 Disemba, 2021 kiasi cha fedha kilichokusanywa ni **Sh. 801,103,993.74** sawa na asilimia **31.43** ya makisio.

**TAARIFA YA UKUSANYAJI WA MAPATO (PERFOMANCE REPORT) KWA MWEZI DESEMBA,2022**

Taarifa ya makusanyo ya mapato kutoka kila Kata (monthry perfomance report) iliwasilishwa ikionesha kiasi cha jumla ya **Tsh. 109,865,290.00** kilikusanywa na wakusanya mapato wote na kati ya hizo kiasi cha **Tsh. 106,690,490.00** ziliwasilishwa benki kwa mwezi Novemba hivyo kufanya jumla ya madeni mapya na ya nyuma kwa wakusanya mapato ni **TSh.170,212,403.23**

**Mjadala;**

Wajumbe wakijadili walishauri yafuatayo;-

- Timu ya mapato ifanye kazi kwa kushirikisha vyombo vingine kama vile Polisi.
- Ushuru wa mazao unatakiwa kutozwa yanapotoka mazao.
- Ushuru wa michezo ya kubahatisha ufuatiliaji ufanyike kwa kila kijiji ili kuongeza
- Halmashauri kuweka utaratibu mzuri wa utoaji wa miche bora inayozalishwa na TACRI ili kudhibiti upotevu wa mapato yatokananayo na mauzo ya miche. Hivyo TACRI wakizalisha wakabidhi kitalu kwa Halmashauri ili igawe kwa utaratibu wake.

**MUHT.NA.KF/MBZ/06/01/2022:- MAPOKEZI YA FEDHA ZA HALMASHAURI KWA MWEZI DISEMBA, 2021**

Ilisomwa kuwa kwa mwezi Disemba, 2021 Halmashauri ilipokea fedha jumla ya **Sh. 819,778,649.32** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo.

**TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA DECEMBA 2021**

| IDARA | OC PROPER | ON CALL | MIRADI YA MAENDELEO | GPG | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| KILIMO | 1,228,416.66 | | | | 1,228,416.66 |
| MIFUGO | 1,068,916.66 | | | | 1,068,916.66 |
| UJENZI | 1,509,583.33 | - | | | 1,509,583.33 |
| AFYA | 10,667,250.00 | 3,449,166.66 | | | 14,116,416.66 |
| ELIMU MSINGI | 3,348,750.00 | | | | 3,348,750.00 |
| ELIMU SEKONDARI | 3,348,750.00 | | | | 3,348,750.00 |
| UCHAGUZI | | | | | - |
| UTAWALA 20% YA VIJIJI | - | | | 1,804,786.40 | 1,804,786.40 |
| UTAWALA | 400,000.00 | | | 600,000.00 | 1,000,000.00 |
| MIPANGO | 400,000.00 | | | 617,529.01 | 1,017,529.01 |
| FEDHA NA BIASHARA | 577,916.66 | | | 703,401.57 | 1,281,318.23 |
| UGAVI | | | | 340,586.62 | 340,586.62 |
| TEHAMA | | | | 340,586.62 | 340,586.62 |
| DCDO | | | - | 513,054.90 | 513,054.90 |
| ARDHI NA MALI ASILI | | | | | - |
| MAZINGIRA | | | | 456,500.00 | 456,500.00 |
| SHERIA | | | | 456,500.00 | 456,500.00 |
| UKAZI WA NDANI | 500,000.00 | | | 513,054.90 | 1,013,054.90 |
| NYUKI | 600,000.00 | | | 281,952.59 | 881,952.59 |
| JUMLA (A) | 23,649,583.31 | 3,449,166.66 | - | 6,627,952.61 | 33,726,702.58 |
| MIRADI YA MAENDELEO | | | - | | - |
| UNICEF | | | 72,650,750.00 | | 72,650,750.00 |
| MFUKO WA JIMBO | | | 100,071,000.00 | | 100,071,000.00 |
| BASKET FUND | | | 180,679,783.13 | | 180,679,783.13 |
| TASAF | | | 241,520,730.00 | | 241,520,730.00 |
| ELIMU BURE MSINGI | | | 104,834,987.10 | | 104,834,987.10 |
| ELIMU BURE SEKONDARI | | | 86,294,696.51 | | 86,294,696.51 |
| JUMLA MIRADI(B) | - | - | 786,051,946.74 | - | 786,051,946.74 |
| **JUMLA KUU(A+B)** | **23,649,583.31** | **3,449,166.66** | **786,051,946.74** | **6,627,952.61** | **819,778,649.32** |

**Mjadala**

Wakijadili wajumbe walishauri kwamba akaunti za vijiji na kata zihuwishwe ili kuwezesha kupokea fedha za rudhuku ya fidia ya vyanzo vilivyofutwa zinazotolewa na Serikali Kuu.

Wajumbe walipokea taarifa ya mapokezi ya fedha kwa mwezi Desemba, 2021 iliyowasilishwa na kuiridhia.

**MUHT.NA.KF/MBZ/07/01/2022:- TATHIMINI YA ZIARA YA KAMATI YA FEDHA, MIPANGO NA UONGOZI.**

Tathimini ya Ziara ya Kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi kukagua miradi ya maendeleo iliyofanyika kuanzia tarehe 28.12.2021, mpaka tarehe 30.12.2021 iliwasilishwa ikiwa na Malengo mahususi yafuatayo:-

i. Kukagua shughuli za miradi ya maendeleo ngazi ya Kata na vijiji
ii. Kupokea kero kutoka kwa Wananchi.
iii. Kuhamasisha Jamii kujiunga na Mfuko wa Afya wa Jamii (iCHF)
iv. Kuhamasisha jamii kutoa ushirikiano katika ukusanyaji wa mapato.
v. Kuhamasisha utekelezaji wa kampeni ya usafi wa mazingira na kujenga vyoo bora ngazi ya kaya na taasisi

**Mjadala**

Wakijadili Wajumbe walishauri maelekezo kutolewa kwa Viongozi wote ngazi za chini wenye miradi ili kuondoa mapungufu yanayobainika na kucheleweshа mradi kukamilika. Aidha wajumbe walishauri Miongozo inayotolewa kuhusu usimamizi wa miradi wah. Madiwani washishirikishwe.

**MAAZIMIO;**

- Ukaguzi ufanyike kwenye miradi yote ya UVIKO 19 ili kupata thamani halisi ya fedha zilizotumika kwa kila mradi.
- Taarifa ya takwimu ya vifaa vilivyobaki pamoja na fedha zilizobaki kwenye miradi ya UVIKO iandaliwe.
- Tathimini ya gharama ya ukamilishaji wa miradi ya Shule ya Sekondari Shikula na Shaji iandaliwe ili Halmashauri isaidie umaliziaji.

**MUHT.NA.KF/MBZ/08/01/2021;- TAARIFA YA MKAGUZI WA NDANI ROBO YA PILI 2021/2022**

**Utekelezaji wa mpango wa ukaguzi kwa robo ya pili kwa mwaka 2021/2022**

Ilisomwa kuwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani katika mpango wake wa ukaguzi kwa robo ya pili kwa mwaka 2021/2022 kilipanga kufanya ukaguzi katika maeneo 9 kimefanikiwa kufanya ukaguzi katika maeneo 7 sawa na asilimia 78 na hakikuweza kufanya ukaguzi katika eneo 2 sawa na asilimia 22.

**Changamoto zilizopelekea kushindwa kufikia asilima 100 ya Mpango wa Ukaguzi kwa robo ya kwanza ya mwaka 2021/2022.**

- Kutolewa kwa kazi na maagizo mengi kutoka Mamlaka za juu ambazo haziko kwenye Mpango wa Ukaguzi.
- Ukosefu au ucheleweshaji wa utolewaji fedha katika kutekeleza shughuli zilizopangwa.
- Uchache wa watumishi katika kitengo cha ukaguzi.
- Kutokuwepo na uelewa wa mifumo (MUSE na GoT Homise).

**Utekelezaji wa hoja za Mkaguzi kwa kipindi cha nyuma au kaguzi zilizopita**
Ilisomwa kuwa Mkaguzi ameangalia mwenendo wa utekelezaji wa mapendekezo ya hoja za Ukaguzi wa ndani zilizotolewa katika robo zilizopita ambazo zilikuwa hazijafungwa, ilisomwa kuwa kulikuwa na hoja 25 hoja 12 sawa na (48%) zimejibiwa na kuweza kufungwa, hoja 13 sawa na asilimia 52% unasubiriwa utekelezaji wa menejimenti.

**YALIYOJITOKEZA KATIKA UKAGUZI ROBO YA KWANZA 2021/2022**
Ilielezwa kwamba katika ukaguzi wa robo ya pili kwa mwaka 201/2022 jumla ya hoja 11 zilitolewa kati ya hizo hoja 2 sawa na 18% zimejibiwa kikamilifu na kuweza kufungwa hoja 6 sawa na 55% hazijafungwa kwakuwa zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama zilivyoainishwa katika jedwali.

**Mjadala;**
Wajumbe walishauri kuwa mkaguzi wa ndani ajiridhishwe kwenye miradi ya shule ya Sekondari Nzovu na Simbega. Pia kwenye maeneo ambayo miradi haijakamilika kama vile kata ya Iyula.

**Azimio;**
- Ukaguzi na ufuatiliaji ufanyike katika mradi wa ukamilishaji vyumba viwili (2) vya madarasa shule ya Msingi Nswiga ambao haujakamilika na taarifa iwasilishwe kikaoni.

Wajumbe walipokea taarifa ya Mkaguzi wa Ndani robo ya pili 2021/2022 iliyowasilishwa na kuridhia

**MUHT.NA.KF/MBZ/09/01/2022 TAARIFA YA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA PILI 2021/2022**
Ilisomwa kuwa katika Kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri iliidhinishwa **Sh. 11,273,762,555** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kuanzia Julai 2021 hadi tarehe 31 Disemba, 2021 Halmashauri imepokea **Sh.3,438,982,731** sawa na asilimia **30** ya Bajeti. Ambapo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ilikuwa na salio anzia la **Sh. 142,418,854.40** hivyo kufanya jumla ya mapokezi na salio anzia ni **Sh.3,581,401,585.68** Matumizi hadi tarehe 31 Disemba, 2021 ni **2,110,295,897** pamoja na salio anzia.
Pia, ilielezwa kwamba katika Mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashari imepokea fedha nje ya bajeti jumla ya sh 3,688,866,578 Matumizi ya fedha hizo mpaka Desemba 31 ni sh 2,589,547,565 ambayo ni sawa na 70% ya fedha iliyopokelewa.

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA ROBO YA II KUANZIA JULAI,2021 HADI TAREHE 31 DISEMBA, 2022.**

| Na. | IDARA | JINA LA MRADI | HALI YA UTEKELEZAJI | (%) YA UTEKELEZAJI | FEDHA ILIYOPOKEWA KUANZIA JULAI, 2021 HADI DISEMBA, 2021 | FEDHA ILIYOTUMIKA KUANZIA JULAI, 2021 HADI DISEMBA, 2021 | CHANZO CHA FEDHA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MIFUGO NA UVUVI | Ujenzi wa Josho katika kijiji cha Bara | Shughuli ya ujenzi zinaendelea | 97 | 18,000,000 | 15,883,333 | Fedha toka serikali kuu |
| | MIFUGO NA UVUVI | Ujenzi wa Josho katika kijiji cha Bara | Shughuli ya ujenzi zinaendelea | 97 | 18,000,000 | 15,883,333 | Fedha toka serikali kuu |
| | | | | | 36,000,000 | **31,766,666** | |
| 2 | ELIMU MSINGI | Ujenzi wa choo matundu 6 shule ya msingi Lutumbi ifikapo Juni, 2022 | Kazi imekamilika | **100** | 6,600,000 | 6,600,000 | EP4R |
| 3 | ELIMU MSINGI | Ujenzi wa choo matundu 6 shule ya msingi Vwawa, | Ujenzi wa matundu 7upo kwenye hatua ya kuweka gypsum | 95 | 6,600,000 | 6,600,000 | EP4R |
| 4 | ELIMU MSINGI | Ujenzi wa choo matundu 6 shule ya msingi Isandula | kazi ya kuchimba shimo inaendelea | 100 | 6,600,000 | 6,600,000 | EP4R |
| 5 | ELIMU MSINGI | Ujenzi wa choo matundu 6 na vyumba 2 vya madarasa Shule ya Msingi Mpela | Ujenzi unaendelea | 75 | 46,600,000 | 28,600,000 | EP4R |
| | | | | | **66,400,000** | **48,400,000** | |
| 6 | ELIMU MSINGI | Ujenzi wa vyoo matundu 29 shule ya msingi Masangula ifikapo Juni, 2022 | Shughuli za uwekaji wa malumalu na kupaka rangi zinaendelea | 90 | 36,401,126 | 33,441,800 | SWASH |
| 7 | ELIMU MSINGI | Ujenzi wa vyoo matundu 25 shule ya msingi Hezya ifikapo Juni, 2022. | Shughuli za uwekaji wa malumalu na kupaka rangi zinaendelea | **88** | 31,801,126 | 27,848,000 | SWASH |
| 8 | ELIMU MSINGI | Ujenzi wa choo matundu 15 shule ya msingi Myovizi ifikapo Juni, 2022. | Shughuli za uwekaji wa malumalu na kupaka rangi zinaendelea | **95** | 20,401,126 | 19,901,100 | SWASH |
| 9 | ELIMU MSINGI | Ujenzi wa choo matundu 21 shule ya msingi Bara ifikapo Juni, 2022. | Shughuli za uwekaji wa malumalu na kupaka rangi zinaendelea | **85** | 27,201,126 | 20,117,800 | SWASH |
| 10 | ELIMU MSINGI | Ujenzi wa vyoo matundu 10 shule ya msingi Kilimampimbi ifikapo Juni, 2022. | Shughuli za uwekaji wa malumalu na kupaka rangi zinaendelea | **95** | 14,701,126 | 14,000,000 | SWASH |
| 11 | ELIMU MSINGI | Ujenzi wa vyoo shule ya msingi Shiwinga matundu 30 ifikapo Juni, 2022. | Shughuli za uwekaji wa malumalu na kupaka rangi zinaendelea | **92** | 37,701,126 | 36,691,126 | SWASH |
| | | | | | **168,206,753** | **151,999,826** | |
| 12 | AFYA | Ujenzi wa matundu ya vyoo na mfumo wa maji Zahanati ya Karasha | Mashimo ya maji taka mawili yameshachibwa,Msingi wa jengo la choo unaendelea kujengwa | | 36,951,945.00 | - | SRWSSP |
| 13 | AFYA | Ujenzi wa matundu ya vyoo na mfumo wa maji zahanati ya Haraka | Mashimo ya maji taka mawili yameshachibwa,Msingi wa jengo la choo unaendelea kujengwa. | | 37,951,945.00 | 3,345,000 | SRWSSP |
| 14 | AFYA | Ujenzi wa matundu ya vyoo na mfumo wa maji zahanati ya Hezya | Ujenzi hauendelei katika Zahanati ya Hezya | | 37,951,945.00 | - | SRWSSP |
| 15 | AFYA | Ujenzi wa matundu ya vyoo na mfumo wa maji zahanati ya Myovizi | Mashimo ya maji taka mawili yameshachibwa,Msingi wa jengo la choo unaendelea kujengwa | | 28,425,000.00 | 4,560,000 | SRWSSP |
| 16 | AFYA | Ujenzi wa matundu ya | Mashimo ya maji taka | | | - | SRWSSP |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | vyoo na mfumo wa maji zahanati ya Senjele | mawili yameshachibwa | | 29,425,000.00 | | |
| 17 | AFYA | Ujenzi wa matundu ya vyoo na mfumo wa maji zahanati ya Msia | Mashimo ya maji taka mawili yameshachibwa,Msingi wa jengo la choo unaendelea kujengwa | | 37,951,945.00 | - | SRWSSP |
| 18 | AFYA | Ujenzi wa matundu ya vyoo na mfumo wa maji zahanati ya Igamba | Mashimo ya maji taka mawili yameshachibwa,Msingi wa jengo la choo unaendelea kujengwa | | 36,951,941.00 | - | SRWSSP |
| 19 | AFYA | Ujenzi wa matundu ya vyoo na mfumo wa maji zahanati ya Nambinzo | Ujenzi hauendelei katika Zahanati ya Nambinzo | | 36,951,941.00 | - | SRWSSP |
| 20 | AFYA | Ujenzi wa matundu ya vyoo na mfumo wa maji zahanati ya Shitunguru | Mashimo ya maji taka mawili yameshachibwa | | 36,951,941.00 | - | SRWSSP |
| 21 | AFYA | Ujenzi wa matundu ya vyoo na mfumo wa maji zahanati ya Itaka | Mashimo ya maji taka mawili yameshachibwa | | 33,406,945.00 | - | SRWSSP |
| 22 | AFYA | Ujenzi wa matundu ya vyoo na mfumo wa maji zahanati ya Halungu | Ujenzi hauendelei katika Zahanati ya Halungu | | 37,951,945.00 | - | SRWSSP |
| 23 | AFYA | Ujenzi wa matundu ya vyoo na mfumo wa maji zahanati ya Mpera | Mashimo ya maji taka mawili yameshachibwa,Msingi wa jengo la choo unaendelea kujengwa | | 37,951,945.00 | 3,586,000 | SRWSSP |
| 24 | AFYA | Ujenzi wa matundu ya vyoo na mfumo wa maji zahanati ya Iyula | Wanaendelea na mchakato wa ununuzi wa vifaa vya kufungia mfumo wa maji | | 28,425,000.00 | - | SRWSSP |
| | | **JUMLA KUU FEDHA ZA SWASH AFYA** | | | **457,249,438.00** | **11,491,000** | |
| | | | | | | | |
| 25 | AFYA | Kusaidia ujenzi wa kituo cha afya Hezya ifikapo Juni 2021 | Jengo la OPD lipo katika hatua ya kupigwa Kenchi na uchapiaji kwenye vyumba unaendelea | 22 | 250,000,000.00 | 79,414,800.00 | Serikali kuu (TOZO ZA MIAMALA YA SIMU) |
| 26 | AFYA | Kusaidia ujenzi wa kituo cha afya Nambinzo ifikapo Juni 2021 | Jengo la OPD lipo katika hatua ya Msingi | 10 | 250,000,000.00 | 14,436,500.00 | Serikali kuu (TOZO ZA MIAMALA YA SIMU) |
| 27 | ELIMU SEKONDARI | Kusaidia nguvu za wananchi katika ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa shule ya Sekondari Halungu ifikapo Juni, 2022 | Jengo la vyumba 2 vya madarasa limekamilika | 100 | 25,000,000.00 | 25,000,000.00 | Serikali kuu (TOZO ZA MIAMALA YA SIMU) |
| 28 | ELIMU SEKONDARI | Kusaidia nguvu za wananchi katika ujenzi wa vyumba 2 vya madrasa shule ya Sekondari Shaji ifikapo Juni, 2022 | Ukamilishaji wa vyumba 2 umefanyika, aidha chumba cha 3 ukamilishaji wake unaendelea | 100 | 25,000,000.00 | 25,000,000.00 | Serikali kuu (TOZO ZA MIAMALA YA SIMU) |
| 29 | ELIMU SEKONDARI | Kusaidia nguvu za wananchi katika ujenzi wa vyumba 2 vya madrasa shule ya Sekondari Isandula ifikapo Juni, 2022 | Jengo la vyumba 2 vya madarasa limekamilika | 100 | 25,000,000.00 | 25,000,000.00 | Serikali kuu (TOZO ZA MIAMALA YA SIMU) |
| 30 | ELIMU SEKONDARI | Kusaidia nguvu za wananchi katika ujenzi wa vyumba 2 vya | Ujenzi umekamilka | 100 | 12,500,000.00 | 12,500,000.00 | Serikali kuu (TOZO ZA MIAMALA YA |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | madrasa shule ya Sekondari Naiputa ifikapo Juni, 2022 | | | | | SIMU) |
| 31 | ELIMU SEKONDARI | Kusaidia nguvu za wananchi katika ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa shule ya Sekondari Nalyelye ifikapo Juni, 2022 | Ujenzi wa boma umekamilika | 75 | 12,500,000.00 | 11,620,000.00 | Serikali kuu (TOZO ZA MIAMALA YA SIMU) |
| | | | | | **600,000,000.00** | **192,971,300.00** | |
| 32 | ELIMU MSINGI | Ujenzi wa bweni kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu shule ya Msingi Lutumbi | Ujenzi upo katika hatua ya ukamilishaji, aidha hatua ya kujenga gebro na skiming inaendelea | 90 | 80,000,000.00 | 73,356,000 | UVIKO 19 |
| 33 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 5 shule ya sekondari Ilolo | Kazi imekamilka | 100 | 100,000,000.00 | 93,619,960 | UVIKO 19 |
| 34 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 shule ya sekondari Ihanda | Kazi imekamilka | 100 | 60,000,000.00 | 59,743,000 | UVIKO 19 |
| 35 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 shule ya sekondari Shikula | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | 38,999,940 | UVIKO 19 |
| 36 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 shule ya sekondari Nalyelye | Kazi imekamilka | 100 | 60,000,000.00 | 59,257,464 | UVIKO 19 |
| 37 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 shule ya sekondari Kilimampimbi | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | 34,164,200 | UVIKO 19 |
| 38 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 6 shule ya sekondari Bara | Kazi imekamilka | 100 | 120,000,000.00 | 112,000,000 | UVIKO 19 |
| 39 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 shule ya sekondari Nzovu | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | 34,457,874 | UVIKO 19 |
| 40 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madrasa 3 shule ya sekondari Msia | Kazi imekamilka | 100 | 60,000,000.00 | 58,470,560 | UVIKO 19 |
| 41 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madrasa 2 shule ya sekondari Nyimbili | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | 39,257,464 | UVIKO 19 |
| 42 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madrasa 2 shule ya sekondari Nanswilu | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | 30,775,464 | UVIKO 19 |
| 43 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madrasa 2 shule ya sekondari Lwati | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | 36,748,664 | UVIKO 19 |
| 44 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madrasa 4 shule ya sekondari Itaka | Kazi imekamilka | 100 | 80,000,000.00 | 72,858,628 | UVIKO 19 |
| 45 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madrasa 2 shule ya sekondari Iganduka | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | 38,013,000 | UVIKO 19 |
| 46 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madrasa 2 shule ya sekondari Isandula | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | 32,510,964 | UVIKO 19 |
| 47 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madrasa 2 shule ya sekondari J.P Magufuli | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | 36,826,000 | UVIKO 19 |
| 48 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madrasa 2 shule ya sekondari Itepula | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | 32,470,764 | UVIKO 19 |
| 49 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madrasa 2 shule ya sekondari Lumbila | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | 35,526,364 | UVIKO 19 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 50 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madrasa 3 shule ya sekondari Myovizi | Kazi imekamilka | 100 | 60,000,000.00 | | 53,452,345 | UVIKO 19 |
| 51 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madrasa 2 shule ya sekondari Halungu | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | | 39,684,580 | UVIKO 19 |
| 52 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madrasa 3 shule ya sekondari Msankwi | Kazi imekamilka | 100 | 60,000,000.00 | | 54,218,056 | UVIKO 19 |
| 53 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 shule ya sekondari Itumpi | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | | 33,752,964 | UVIKO 19 |
| 54 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 shule ya sekondari Hampangala | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | | 34,457,874 | UVIKO 19 |
| 55 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 shule ya sekondari Ipunga | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | | 39,353,464 | UVIKO 19 |
| 56 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 shule ya sekondari Hezya | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | | 36,478,464 | UVIKO 19 |
| 57 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 shule ya sekondari Idimi | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | | 38,888,764 | UVIKO 19 |
| 58 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 shule ya sekondari Igamba | Kazi imekamilka | 100 | 60,000,000.00 | | 57,579,296 | UVIKO 19 |
| 59 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 5 shule ya sekondari Iganya | Kazi imekamilka | 100 | 100,000,000.00 | | 94,000,000 | UVIKO 19 |
| 60 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 shule ya sekondari Isalalo | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | | 38,851,664 | UVIKO 19 |
| 61 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 5 shule ya sekondari Isangu | Kazi imekamilka | 100 | 100,000,000.00 | | 92,999,160 | UVIKO 19 |
| 62 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 6 shule ya sekondari Kisimani | Kazi imekamilka | 100 | 120,000,000.00 | 112,000,000 | | UVIKO 19 |
| 63 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3shule ya sekondari Mlowo | Kazi imekamilka | 100 | 60,000,000.00 | | 59,412,000 | UVIKO 19 |
| 64 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 shule ya sekondari Mlangali | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | | 38,136,596 | UVIKO 19 |
| 65 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 shule ya sekondari Msangawale | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | | 36,207,564 | UVIKO 19 |
| 66 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 shule ya sekondari Msense | Kazi imekamilka | 100 | 60,000,000.00 | | 59,259,838 | UVIKO 19 |
| 67 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 4 shule ya sekondari Naiputa | Kazi imekamilka | 100 | 80,000,000.00 | | 76,000,000 | UVIKO 19 |
| 68 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 5 shule ya sekondari Nambinzo | Kazi imekamilka | 100 | 100,000,000.00 | | 96,500,000 | UVIKO 19 |
| 69 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 4 shule ya sekondari Nkanga | Kazi imekamilka | 100 | 80,000,000.00 | | 73,867,928 | UVIKO 19 |
| 70 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 shule ya sekondari Ndugu | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | | 38,421,464 | UVIKO 19 |
| 71 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 3 shule ya sekondari Shaji | Kazi imekamilka | 100 | 60,000,000.00 | | 59,731,200 | UVIKO 19 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 72 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 shule ya sekondari Shiwinga | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | 35,441,464 | UVIKO 19 |
| 73 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 2 shule ya sekondari Simbega | Kazi imekamilka | 100 | 40,000,000.00 | 35,441,464 | UVIKO 19 |
| 74 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa vyumba vya madarasa 7 shule ya sekondari Vwawa | Kazi imekamilka | 100 | 140,000,000.00 | 136,985,000 | UVIKO 19 |
| 75 | ELIMU SEKONDARI | Ujenzi wa mfumo wa maji shule ya sekondari Mlowo | Kazi imekamilika | 100 | 11,872,379.85 | 11,872,380 | UVIKO 19 |
| 76 | ELIMU MSINGI | Ujenzi wa mfumo wa maji shule ya sekondari Itete | Kazi imekamilika | 100 | 11,872,379.85 | 11,872,380 | UVIKO 19 |
| 77 | ELIMU MSINGI | Ujenzi wa mfumo wa maji shule ya sekondari Haloli | Kazi imekamilika | 100 | 11,872,379.85 | 11,872,380 | UVIKO 19 |
| | | | | | **2,595,617,139.55** | **2,425,794,599** | |
| 78 | TASAF | Kusaidia kaya 9172 zilizokithiri kwa umasikini | Utekelezaji unaendela | 22 | 557,368,000.00 | 557,368,000.00 | SERIKALI KUU |
| | | | | | **557,368,000.00** | **557,368,000.00** | |

Wajumbe walipokea taarifa ya miradi ya maendeleo kwa robo ya pili kwa mwaka 2021/2022 iliyowasilishwa na kuridhia

**MUHT.NA.KF/MBZ/10/01/2022 TAARIFA YA KITENGO CHA MANUNUZI ROBO YA PILI 2021/2022**

Taarifa tajwa iliwasilishwa kwa wajumbe ikionesha Halmashauri imefanya malipo yenye thamani ya **Tsh. 864,915,469.04** yaliyohusisha manunuzi ya bidhaa mbalimbali, huduma na kazi.

Ununuzi wa bidhaa ulihusika na manunuzi ya vifaa vya ofisi, vifaa vya ujenzi, vipuri vya magari, mafuta ya magari na mitambo na ununuzi wa vyakula kwenye vikao na semina. Aidha, ilielezwa kuwa Halmashauri ina madeni yaliyotokana na manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na 2020/2021 kiasi cha **Tsh. 69,564,756.08** na madeni ya miaka nyuma 2013/2014 hadi 2018/2019 yenye jumla ya **TSh. 370,779346.04**

**Mjadala.**

Wakijadili Wajumbe walishauri kitengo cha manunuzi kuainisha madeni ya nyuma kwa robo mwaka ilikujitathimini namna ya ulipaji ukilinganisha na taarifa ya nyuma.

**Azimio**

- Ufuatiliaji na uhakiki wa nyaraka ufanyike kwa madeni ambayo Halmashauri inayodaiwa ili madeni halali yalipwe likiwepo deni la miche ya miparachichi.

Wajumbe walipokea taarifa ya Kitengo cha Manunuzi kwa robo ya pili ya mwaka 2021/2022 iliyowasilishwa na kuridhia.

**MUHT.NA.KF/MBZ/11/01/2022 TAARIFA YA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASIKINI TASAF ROBO YA PILI 2021/2022**

Ilisomwa kuwa utekelezaji wa shughuli za mpango wa kunusuru kaya masikini sana kwa kipindi cha mwezi Oktoba hadi Disemba, 2021 ni kama ifuatavyo:-

- Kutoa malipo ya Sh. 305,590,000/= kwa kaya 7,953 za walengwa wa kaya maskini sana za TASAF na kaya 43 hazikuhudhuria kupokea fedha Sh. 1,618,000/= kutokana na Vifo, kusafiri, shughuli za kilimo na kuhama makazi kutoka kijiji cha mpango.
- Kuondoa Kaya 12 katika Mpango kutokana na kufariki dunia na kutokuwa na wategemezi watakao endelea kupokea Ruzuku hiyo.
- Kufanya ufuatilia katika Vijiji 21 na kuwakumbusha Walengwa wajibu wao katika mpango wa TASAF katika Vijiji vya Twinzi,Iporoto,Ikonya,Maninga,Itentula,Isela,Hamwelo,Itaka,Shitunguru,Utambalila,Ipapa,Itewe,Shasya,Hasamba,Hantesya,Ilolo,Vwawa,Ichenjezya,Shilanga,Mlowo na Lwati ambapo Walengwa wameweza kuanzisha shughuli mbalimbali za kujiongezea kipato ufugaji Mbuzi 49, kuku 62,Nguruwe17 na Vikundi 6 vya walengwa vimeundwa 3 kijiji cha Itentula na 3 kijiji cha Itaka

Wajumbe walipokea taarifa ya TASAF kwa robo ya pili ya mwaka 2021/2022 iliyowasilishwa na kuridhia.

**MUHT.NA.KF/MBZ/12/01/2022 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA USIMAMIZI WA UDHIBITI WA VIHATARISHI ROBO YA PILI 2021/2022**

Ilisomwa kuwa Mpango wa usimamizi wa udhibiti wa Vihatarishi uliopitishwa katika vikao vya kisheria vilivyofanyika robo ya pili, Januari, 2021 ambavyo ni kikao cha Kamati ya Wakuu wa Idara (CMT), kamati ya Ukaguzi Wilaya (Audit Committee), kamati ya Fedha na Baraza Kamili la Madiwani umeendelea kutekelezwa. Taarifa ya utekelezaji wa Mpango huu kwa robo ya pili, Oktoba hadi Disemba, 2021 iliwasilishwa ilionesha viashiria vya Vihatarishi, hali za utekelezaji na maoni kwa Idara ya Afya, Elimu Sekondari, Utumishi na Utawala, Usafi na Mazingira, Maendeleo ya Jamii, na Manunuzi.

Wajumbe walipokea taarifa ya Utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa udhibiti wa vihatarishi uliowasilishwa na kuridhia.

**MUHT.NA.KF/MBZ/15/01/2022:- TAARIFA YA MAREKEBISHO YA VIFUNGU NDANI YA BAJETI (REALLOCATION WITHIN) KATIKA BAJETI YA MWAKA 2021/2022**

Taarifa tajwa iliwasilishwa kwa wajumbe ikionesha utekelezaji wa Bajeti na Marekebisho ya Vifungu yaliyofanyika ili kuleta ufanisi wa utekelezaji wa Bajeti na uendeshaji wa Halmashauri ambapo jumla ya **Tsh. 768,213,576.98** Zilifanyiwa marekebisho kutoka Idara na Vitengo vya Halmashauri. Ikiwa **Tsh. 298,213,576.98** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Tsh. 470,000,000.00** ni kwa ajili ya Ujenzi wa

shule mpya ya sekondari Ilembo chini ya Mpango wa Kuboresha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP).

**Mjadala;**
Wajumbe wakijadili walishauri kuwa mambo muhimu katika uendeshaji wa Halmashauri yapewe kipaumbele.

Baada ya mjadala wajumbe walipokea na kuridhia taarifa ya marekebisho ya vifungu (Reallocation) iliyowasilishwa

**MUHT.NA.KF/MBZ/16/01/2022:- TAARIFA YA KILA MWEZI**

***i. Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)***

Halmashauri kupitia Idara ya Afya imefanikiwa kusajili kaya 192 zenye jumla ya Wategemezi 931 sawa na Tsh. 5,760,000
Jumla ya kaya 2,813 ziko hai sawa na asilimia 2.3 ya kaya zote 119096 zilizopo Wilaya ya mbozi.

**MAFANIKIO**
Ilielezwa kwamba Halmashauri imefanikiwa kupokea kadi 9,000 kutoka Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa ambazo zinatumika kusajili wateja waliolipiwa na wadau na wengine wanaolipia papo kwa papo.

**MIKAKATI**
- Kuendelea kufanya uhamasishaji kupitia vikundi, na kupita nyumba kwa nyumba kwa kutumia CHWs ambao wapo kwenye maeneo husika na Maafisa waandikishaji.
- Kuendelea kupita na kuhamasisha kwa wadau mbalimbali waweze kuwalipia watu wanaofanya nao kazi,.

Wajumbe walipokea na kuridhia taarifa ya Bima ya Afya iliyoboreshwa (iCHF) kwa robo ya pili iliyowasilishwa.

***ii. VVU na UKIMWI***

Ilisomwa kwamba Halmashauri katika kuhakikisha inatimiza azma ya Serikali ya mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU/UKIMWI kwa kipindi cha mwezi Disemba, 2021 imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za Afua za UKIMWI kwa kushirikiana na Wadau kama ifuatavyo;-
- Kuvijengea uwezo vikundi 17 vya Watu wanaoishi na VVU/UKIMWI kwa kutoa elimu ya mikopo, ujasiliamali na Lishe katika Kata za Nambizo,Mahenje,Bara,Ruanda na Isansa.
- Kutoa elimu ya tohara kwa vijana wa kiume 1769 katika kata za Vwawa, Bara, Nambizo, Ichenjezya, Ilolo, Hasanga, Hasamba Mlowo, Idiwili Na Igamba.
- Ugawaji wa mipira ya kondom 22,400 katika maeneo ya Bar ,Vijana na Watu waishio na VVU/UKIMWI

- Kufanya madhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani tarehe 1/Disemba/2021. Yaliyofanyika Kata ya Hasamba Vwawa

**CHANGAMOTO;**

- Baadhi ya wanachama kupotea katika dawa
- Ukosefu wa Ofisi ya Konga Wilaya .
- Ukosefu wa mitaji kwa baadhi ya vikundi vya watu waishio na VVU/UKIMWI.

**MAFANIKIO;**

- Kupitia mawakili tiba baadhi ya waliopotea katika dawa wameweza kurejeshwa.
- Kupitia mapato ya ndani kwa robo hii vikundi viwili vimefanikiwa kupewa mkopo utakao wasaidia kuimalisha kipato na afya za familia.

Wajumbe walipokea taarifa ya utekelezaji Afua za mapambano ya maambukizi ya VVU/UKIMWI iliyowasilishwa na kuridhia.

***iii. Utekelezaji wa shughuli za Idara ya Utawala na Utumishi.***

Taarifa ya Shughuli zilizotekelezwa na Idara ya Utawala na Utumishi kwa kipindi cha mwezi Disemba, 2021, iliwasilishwa kikaoni ikionesha kazi zilizofanyika ni pamoja na kusimamia maslahi ya Watumishi ikiwemo Mishahara na kupandishwa Vyeo. Yafuatayo ni Mafanikio yaliyopatikana :-

- Idara imesimamia vyema maslahi ya watumishi ikiwemo upandishaji vyeo na maandalizi ya mishahara kwa wakati. Jumla ya watumishi 3907 wamelipwa mishahara.
- Vikao 3 vya kisheria ikiwa Kamati ya Wakuu wa Idaya, Kamati ya Fedha na Mkutano wa Baraza Maalum la Madiwani vimefanyika kwa mwezi Disemba, 2021 katika kuimarisha Utawala bora.
- Watumishi 9 wamehama kutoka Halmashauri ya Mbozi kwenda Halmashauri mbalimbali na
- Watumishi 6 wamehamia kutoka Halmashauri mbalimbali .
- Halmashauri inao jumla ya Watumishi **3907** kati ya hitaji la watumishi **5503** na kwamba inaupungufu wa watumishi **1596.**

Wajumbe walipokea taarifa ya Idara ya Utawala na Utumishi iliyowasilishwa na kuridhia.

**MUHT.NA. KF/MBZ/17/01/2022:- TAARIFA ZA MKURUGENZI**

**i. Taarifa za ununuzi wa Mitambo**

Ilielezwa kwamba kufuatia kusudio la Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kununua mtambo wa kutengeneza barabara (Grader) ikiwa na lengo la kuongeza mapato ya ndani ya Halmashauri na kuboresha huduma za kijamii na kiuchumi. Pamoja na maoni ya kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira katika kikao cha tarehe 18.01.2022 kilichoshauri fedha zilizotengwa kwa ajili ya uchimbaji mabwawa na ununuzi wa bati zitumike katika manunuzi ya mtambo wa ujenzi (Excavators).

Mapendekezo ya kununua mtambo (Excavators) yaliwasilishwa yakionesha aina ya mtambo na bei yake kisha kuwasilisha kwa Wajumbe.

| Na | MAELEZO | | GHARAMA | |
|---|---|---|---|---|
| | | QTY | $ | Tsh |
| 1. | 320 New CAT Excavators | 1 | 177,000.00 | 408,162,000.00 |
| 2. | New Hyundai Crawler Excavator Model R220LS | 1 | 130,000.00 | 299,780,000.00 |

**Mjadala**

Wakijadili wajumbe waliridhia mapendekezo ya Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya uchimbaji mabwawa na ununuzi wa bati ziondolewe na kutumika kuongeza fedha za ununuzi wa mtambo wa ujenzi.

**Azimio;**

- Taratibu za manunuzi ziendelee ili Halmashauri inunue mtambo wa ujenzi (Excavators )

**MUHT.NA. KF/MBZ/18/01/2021:- KUFUNGA KIKAO**

Akifunga kikao Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa ushiriki wao kikaoni.
Baada ya maelezo hayo alifunga kikao rasmi saa 7:02 Mchana.

***= UMETHIBITISHWA =***

| | | |
|---|---|---|
| ............ | 18/02/2022 | ............ |
| *George J. Musyani* | ***Tarehe*** | *Abdallah H. Nandonde* |
| ***Mwenyekiti*** | | ***Katibu*** |